



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Kumb.Na.BA.1/25/01A/28

05 Mei, 2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi ya kazi kwa ajili ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kama ifuatavyo:-

1. Mhasibu Daraja la II (ZPSG-) Nafasi 4 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu Shahada ya kwanza katika fani ya Uhasibu au Usimamizi wa Fedha au Usimamizi wa Biashara (akiwa amejikita katika Fani ya Uhasibu) au Uhasibu na Fedha au Usimamizi wa Fedha na Uwekezaji au Teknolojia ya habari na Uhasibu au Usimamizi wa Benki na Fedha kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Muombaji mwenye CPA au IPSAS au cheti kinacholingana na hizo atapewa kipa umbele.

2. Mhasibu Msaidizi Daraja la III (ZPSE-03) Nafasi 7 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu Stashahada ya Kawaida (Ordinary Diploma) ya Usimamizi wa Fedha au Usimamizi wa Biashara (Akiwa amejikita katika Fani ya Uhasibu au Fedha) au Uhasibu na Fedha au Usimamizi wa Fedha na Uwekezaji au Teknolojia ya Habari na Uhasibu au Usimamizi wa Benki na Fedha kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

3. Afisa Kumbukumbu Daraja la II (ZPSG-10) Nafasi 1 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu Shahada ya kwanza katika fani ya Utunzaji kumbukumbu na Nyaraka (Records Management and Archives) au fani inayohusiana na Teknolojia ya Usimamizi wa Taarifa (Data) /kumbu kumbu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar.

4. Afisa Kumbukumbu Msaidizi Daraja la III (ZPSG-02) Nafasi 1 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu Stashahada katika fani ya Usimamizi wa kumbukumbu (Records Management) kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

5. Afisa Utumishi Msaidizi Daraja la III (ZPSE-03) Nafasi 1 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka 46.
- Awe amehitimu Stashahada katika fani ya Usimamizi wa Rasilimali watu au Utawala na Usimamizi wa Ofisi kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

6. Dereva Daraja la III (ZPSE-04) Nafasi 1 – Unguja

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne na Kupata cheti cha Mafunzo ya Udereva kutoka katika Chuo kinachotambulika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na leseni hai ya Udereva kuanzia Class C na kuendelea.

Jinsi ya Kuomba:

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: <https://portal.zanajira.go.tz> kuanzia tarehe **05 Mei, 2026** hadi tarehe **19 Mei, 2026**.
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini www.zanajira.go.tz.
- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-
**KATIBU,
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,
S.L.P 1587,
ZANZIBAR**
- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoomba.
- Muombaji atakaewasilisha “Progressive Report” au “Statement of Results” pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:
KATIBU,
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.
ZANZIBAR**